

HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI

SHULE YA SEKONDARI NKUU,

S.L.P 7750,

MOSHI.

MOB: 0767 117 757

TAREHE:

Kumb.Na.NSS/F.1 2021/Vol.1/26

Jina la mwanafunzi.....

.....

S.L.P.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NKUU WILAYA YA HAI MKOA WA KILIMANJARO MWAKA 2021.

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha I katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari Nkuu ipo eneo la Kimbushi, kijiji cha Nkuundoo, kata ya Machame-Mashariki, Tarafa ya Lyamungo. Shule yetu ni ya kutwa na yenye mchanganyiko wa wasichana na wavulana.

Muhula wa kwanza wa masomo unanza tarehe 11/01/2021, unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2021. Endapo shule haitapokea taarifa yoyote juu yako hadi tarehe hiyo utahesabiwa kuwa kati ya wale wasio na mpango wa kujiunga na shule hii.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA/KUANDAA

2.1 (a)Sare za shule hii ni:-

Wavulana: suruali mbili rangi ya maroon, mashati mawili meupe tetron mikono mifupi, sweta moja rangi kama ya suruali, soksi nyeupe (pair mbili) na viatu vyeusi vya ngozi(vya kamba)

Wasichana: Sketi mbili rangi ya maroon, blauzi mbili nyeupe tetron mikono mifupi, sweta moja rangi kama ya sketi, soksi nyeupe(stocking pair mbili) na viatu vyeusi vya ngozi(vya kamba) vya kutumbukiza-visigino vifupi. Maelezo ya mshono yapo kwa mafundi jirani na Ofisi za kijiji cha Nkuusinde, unashauriwa kuomba ushauri kwao

ingawa hulazimishwi kushona sare hiyo hapo. **Utapewa kipande cha kitambaa kwa ajili ya suruali/sketi na sweta.**

(b). Rangi ya hijabu ifanane na mashati ya shule

(c) .Sare za michezo kwa kidato cha kwanza ni T-sheti na bukta (rangi ya bluu) kwa wavulana na kwa wasichana ni truck suit & T-shirt rangi ya bluu.

2.2. Mwanafunzi awe na daftari (counter book quire 2) 10 kwa masomo yote,

kalamu,mkebe wa vifaa hisabati(mathematical set) na kamusi ya kingereza(oxford)

2.3. Utaratibu wa chakula cha mchana kwa wanafunzi, wazazi washaweka makubaliono na

kuunda kamati ya usimamizi na uendeshaji, ambayo ndiyo hutoa maelezo ya namna ya uendeshaji wa zoezi chakula shuleni.

3.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sharia Elimu na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sharia Na.10 ya mwaka 1995, aidha inazingatia miongozo yote iliyotolewa na wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Raisi-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na endeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

- i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
- ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- iii. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni(preparation/remedial)
- iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

ix. Kutunza mali za umma.

3.1. Makosa yafuatayo yanaweza kukusababisha kufukunzwa au kusimamishwa shule.

- a. Wizi
- b. Uasherati na ushoga
- c. Ubakaji
- d. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyo kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kuberi na kadharika.
- e. Kupiga au kupigana
- f. Kuharibu kwa makusudi mali za umma
- g. Kudharau bendera ya taifa
- h. Kupata mimba/kuwa mjamzito
- i. Kuoja au kuolewa
- j. Kutoa mimba
- k. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule
- l. Kukataa adhabu kwa makusudi
- m. Kuwa na simu ya mkononi.

4.0. Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.

- a) Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikari. Fomu hii itakabiziwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- c) Fomu ya mzazi kukuri kukubaliana na sharia, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule

5.0 Tafadhari soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBUNI SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI NKUU

.....

**ESTER J. HAYUMA
MKUU WA SHULE**

SHULE YA SEKONDARI NKUU

AHADI YA KUKUBALI NAFASI NILIYOPATA

A. SEHEMU YA MWANAFUNZI

Mimi nakubali kupokea nafasi hii ya masomo katika shule ya sekondari Nkuu. Naahidi kuwa nitatii sheria zote za shule, nitakuwa mwaminifu, nitajitahidi kujifunza kwa bidii kwa kadili ya uwezo wangu na kufanya kazi nyingine zote nitakazopangiwa kwa juhudi na maarifa. Nitafika shuleni siku zote na masomo bila kuchelewa. **Kushindwa kwangu kutii ahadi hii kanuni na sheria za shule zichukue mkondo wakae.**

Saini ya mwanafunzi:
Anuani ya nyumbani:
.....
.....

B. SEHEMU YA MZAZI/MLEZI(AHADI)

Miminimekubali kumpatia mwanana(jina la mwanafunzi)mahitaji muhimu ya shule (sare za shule,vifaa vingine na daftari) ili aweze kusoma na kujifunza bila matatizo. Naahidi kushirikiana na walimu katika kumlea mwanangu kadri ya uwezo wangu.

SAINI YA MZAZI/MLEZI.....
ANUANI
.....
.....
SIMU

SHULE YA SEKONDARI NKUU

TAARIFA ZA MWANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi.....
2. Shule ya msingi uliyotoka:.....
3. Uraia.....
4. Dini:.....Dhehebu.....
5. Kuzaliwa: tarehemwezi.....mwaka.....
6. Ulikozaliwa : kijijikitongoji.....wilaya.....
7. Jina la baba mzazi.....
8. Anuani ya nyumba.....simu.....
9. Kazi ya baba/mlezi.....
10. Kazi ya mama.....
11. Je una udhaifu wa kimaumbile(ulemavu).....
12. Balozi wako.....
13. Mwenyekiti wa kitongoji.....
14. Mengineyo
.....
.....
.....
.....
.....
- .
Saini ya mwanafunzi.....
- Tarehe.....

NKUU SECONDARY SCHOOL
MEDICAL EXAMINATION FORM

This form should be field by a medical officer

FULL NAME.....

AGE.....

BLOOD ACCOUNT (RED&WHITE)

STOOL.....

URINE.....

V.D.....

T.B.....

EYES.....

EARS.....

TEETH.....

SKIN TREATMENT GIVEN(IF ANY).....

ABDOMEN.....

HEART.....

PREGNANT TEST(FOR GIRLS).....

ANY ADDITIONAL INFORMATION e.g physical defects, infections, impairments and
any other abnormalities

.....

.....

.....

I certify that the above examinee is fit

SIGNATURE.....

OFFICIAL STAMP.....

DATE.....